

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**WAJUMBE WA KONGAMANO LA MISRI WAKUBALIANA KUKUZA
UCHUMI LICHA YA COVID 19**

Wajumbe wa Kongamano la Kimataifa la Ushirikiano la Misri (Egypt International Cooperation Forum) ikiwemo Tanzania wamekubaliana kutoa ripoti ya tathimini ya mkutano huo baada ya miezi mitatu ambapo yote yaliyojadiliwa na kukubaliwa likiwemo suala la kuendeleza ukuaji wa uchumi licha ya changamoto ya Covid 19 yatatolewa mwongozo kwa ajili ya utekelezaji.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba wakati wa kuhitimisha Kongamano la Kimataifa la Ushirikiano la Misri (Egypt International Cooperation Forum) lililofanyika kwa siku mbili mjini Cairo nchini Misri.

Dkt. Nchemba alisema kongamano hilo limemalizika na ajenda mbalimbali zilijadiliwa zikiwemo za mikakati ya kupambana na Uviko- 19 na umuhimu wa mahusiano ya kimataifa katika kujijenga kiuchumi.

Katika hatua nyingine Dkt. Nchemba alitembelea ofisi za ubalozi wa Tanzania nchini Misri ambapo alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Tanzania nchini Misri Mhe. Meja Jenerali Anselm Bahati.

Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mhe. Daniel Sillo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Bi. Amina Khamis Shaaban na wataalamu kutoka wizara hiyo.

Imetolewa na:

**Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha ya Mipango**